# KANUNI ZA MAADILI YA WAANDISHI WA HABARI

Toleo la 2020

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

BARAZA LA HABARI TANZANIA (MCT)

# KANUNI ZA MAADILI YA WAANDISHI WA HABARI

Toleo 2020

# KANUNI ZA MAADILI YA WAANDISHI WA HABARI

**© Baraza la Habari Tanzania, 2020**

**ISBN:** 978 - 9987 - 710 - 95 - 9

## YALIYOMO


Utangulizi ....................................................................................................1

SURA YA KWANZA.........................................................................................5

MISINGI INAYOTUMIKA KWA WAANDISHI WA HABARI WA VYOMBO VYA HABARI VYA MAGAZETI, REDIO, TELEVISHENI NA VYOMBO VYA HABARI MTANDAONI. ..........................5

1.0 Ukweli ....................................................................................................5
2.0 Uhuru na mgongono wa maslahi ..........................................................5
3.0 Wajibu na uwajibikaji .............................................................................6
4.0 Uaminifu na weledi wa vyombo vya habari...........................................6
5.0 Usahihi, uhakiki ......................................................................................6
6.0 Haki na usawa........................................................................................7
7.0 Haki ya kujibu .........................................................................................7
8.0 Masahihisho ...........................................................................................7
9.0 Habari za uongo .....................................................................................8
10.0 Dhana ya kutokuwa na hatia ...............................................................8
11.0 Kupunguza madhara..............................................................................8
12.0 Vyanzo vya habari visivyokuwa na jina ................................................9
13.0 Kutotangaza vyanzo vya habari ............................................................9
14.0 Ukweli na maoni .....................................................................................9
15.0 Kurekodi mahojiano na mazungumzo kwa njia ya simu ......................9
16.0 Kuheshimu faragha na utu wa mtu.......................................................9
17.0 Uingiliaji wakati wa majonzi na mshituko ............................................10
18.0 Kuripoti migogoro ya kikabila na kidini..................................................10
19.0 Sifa na utu ...............................................................................................11
20.0 Uzingatiaji jinsia.......................................................................................11
21.0 Utoaji habari za watu wenye ulemavu na makundi yaliyo katika mazingira magumu11
22.0 Maneno machafu, utashi na jinsi ya utoaji taarifa.................................12
23.0 Matumizi ya picha na majina ..................................................................12
24.0 Kuwalinda Watoto.....................................................................................12
25.0 Ubaguzi na kauli za chuki.........................................................................13
26.0 Vurugu na maudhui ya michoro...............................................................13
27.0 Ndugu na marafiki wasio na hatia ..........................................................14
28.0 Uchochezi wa ugomvi ...............................................................................14
29.0 Vitendo vya rushwa ...................................................................................14
30.0 Wizi wa maandishi ......................................................................................15
31.0 Matangazo. ..................................................................................................15
32.0 Utaratibu wa kupata maoni .......................................................................15

SURA YA PILI ........................................................................................................16

MISINGI INAYOTUMIKA KWA WAANDISHI WA HABARI WA VYOMBO VYA HABARI VYA UTANGAZAJI TU .......................................................................................................16

1.0. Mahojiano ..................................................................................................16

2.0. Vipindi mbashara vya kupiga simu ........ 16
3.0. Njia ya udhibiti na nidhamu ........ 17
4.0. Upangiliaji ........ 17
5.0. Vipindi vya watoto ........ 17
6.0. Usalama ........ 18
7.0. Tahadhari kwa maudhui yasiyopendeza, yanayochukiza na yenye mashambulizi 19
8.0. Uhariri na viwango vya utayarishaji ........ 19
9.0. Masuala ya utata yenye umuhimu kwa umma ........ 19
10.0. Vibonzo ........ 19
11.0. Uchaguzi na kura ya maoni ........ 20
12.0. Ushindani kwa ajili ya usawa ........ 20
13.0. Matangazo ya biashara ........ 20
14.0. Uhakikisho na zawadi ........ 21
15.0. Kilevi, tumbaku, usalama wa barabarani na masuala ya mazingira ........ 21
16.0. Uwasilishaji ........ 21
17.0. Mashindano ........ 21
18.0. Udhamini ........ 21
19.0. Uchambuzi, maelezo na tahariri ........ 22
20.0. Maudhui yaliyoandaliwa kwa mtumiaji kutangazwa kwenye televisheni au redio 22
21.0. Matumizi ya maudhui ya wengine kutoka kwenye mitandao au yaliyotolewa na umma. ........ 23
22.0. Matukio ya jukwaani ........ 24

**SURA YA TATU ........ 25**
**MISINGI INAYOTUMIKA KWA WATAYARISHAJI WA MAUDHUI YA MITANDAONI ........ 25**
1.0. Maudhui kutoka kwa mtumiaji ........ 25
2.0. Taratibu za taarifa na uchukuaji wa hatua ........ 26
3.0. Matumizi ya taarifa ya mtu wa tatu kutoka kwenye mitandao ya kijamii au iliyotoka kwa umma ........ 27
4.0. Maoni/mrejesho ........ 28
5.0. Uondoaji au uzuiaji wa maudhui ........ 28
6.0. Hakimiliki ........ 28
7.0. Wizi wa maandishi ........ 28
8.0. Kutaja chanzo ........ 28
9.0. Kulinda haki ya maudhui ........ 29
10.0. Kulinda faragha ya maudhui ........ 29
11.0. Nyaraka za mtandaoni, uchapishaji tena maudhui ya mtu mwingine ........ 29
12.0. Utangazaji biashara mtandaoni ........ 30
13.0. Kanusho ........ 30

**SURA YA NNE ........ 31**
**MISINGI INAYOTUMIKA KWA WAMILIKI WA VYOMBO VYA HABARI NA WACHAPISHAJI ........ 31**
1.0. Uhuru ........ 31

2.0. Usalama na muda wa ajira ........ 31
3.0. Msukumo usio wa lazima au ushawishi ........ 31
4.0. Unyanyasaji wa kijinsia ........ 31
5.0. Kulipia taarifa ........ 32
6.0. Mgongano wa maslahi ........ 32
7.0. Weledi wa kitaaluma ........ 32
8.0. Nguvu au vitisho ........ 32
9.0. Kurudisha fadhila kwa jamii ........ 32
10.0. Uchunguzi ........ 33
**MAREJEO** ........ **34**

# UTANGULIZI

Msingi wa demokrasia imara unatokana na uwepo wa vyombo huru vya habari vinavyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia weledi na uwajibikaji. Vyombo hivyo vya habari huwezesha uchunguzi makini wa masuala yanayoihusu jamii na hivyo ni muhimu katika kuona demokrasia inafanikiwa ndani ya jamii. Wajibu muhimu zaidi wa vyombo vya habari ni kwa umma na ni lazima viwajibike kwao. Vilevile huwawezesha wananchi kufurahia haki yao ya kupata habari na kutoa maoni kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania1, 1977.

Ibara ya 18 ya Katiba hiyo inasema kuwa: Kila mtu (a) anao uhuru wa kuwa na kueleza fikra zake, (b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi, (c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; na (d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Vyombo vya habari vinajitahidi kuzitekeleza haki hizi kwa uaminifu kwa ajili ya wananchi, na kazi yake daima inaongozwa na maslahi kwa umma, inayofahamika kwa kutoa taarifa muhimu na kuzingatia maslahi ya jamii. Waandishi wa habari ni lazima wazingatie viwango vya hali ya juu vya kudumisha uaminifu na kutunza imani yake kwa umma. Hii ina maana kwamba mara kwa mara kusimamia ukweli, kujiepusha na madhara yasiyokuwa ya lazima kwa jamii, kuzingatia maoni na sauti za watu wenye mitazamo tofauti katika uandishi wetu kwenye matukio mbalimbali, kuonyesha uzingatifu katika uandishi habari za watoto na makundi yaliyo kwenye mazingira hatarishi na kutangaza umuhimu wa mila, tamaduni na desturi za wasomaji na mada wanazozitolea taarifa, na kufanya kazi kwa uhuru.

Kanuni hizi zinaweka msingi wa viwango vya misingi inayotakiwa. Kwa ujumla zinalinda haki za watu na kuzingatia matakwa ya umma ya kupashwa habari.

Aidha, kanuni hizi ni msingi wa mfumo wa kujisimamia ambao tasnia ya habari imekubaliana kuendelea kuutekeleza. Kanuni hizi pia ni marejeo kwa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari (MCT) inapokuwa ni lazima kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mwanachama yeyote anayekiuka maadili husika. Ni wajibu wa wahariri, wachapishaji na watangazaji kushirikiana na Baraza la Habari kuhakikisha uamuzi wa

haraka wa malalamiko.

Kanuni hizi zimekusudiwa kuhakikisha kuwa wanachama wanazingatia viwango vya juu vya kimaadili, weledi na mwenendo mzuri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wahariri, wachapishaji na watangazaji wanapaswa kuhakikisha kuwa kanuni hizi zinatumiwa na si tu wafanyakazi wao, bali pia yeyote anayechangia katika machapisho au matangazo yao. Ni muhimu kwa wahariri na waandishi wa habari wakazingatia utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia kanuni hizi sambamba na kuziheshimu.

Kanuni hizi zisitafsiriwe juujuu na kuathiri dhamira yake ya kuheshimu haki za mtu kiasi cha kutochapisha au kutangaza jambo lenye maslahi ya umma.

Kanuni hizi za maadili zitawahusu wafuatao: mwandishi binafsi, waandishi wa safu, wachora vibonzo, watangazaji, wapigapicha, watengenezaji wa video, mameneja wa vyombo vya habari na wahariri (ambao kwa kanuni hizi wataitwa wafanyakazi wa vyombo vya habari). Wengine wanaohusika na kanuni hizi ni wamiliki wa vyombo vya habari, wachapishaji na watayarishaji wa maudhui mitandaoni.

Kanuni hizi zina sura nne, Sura ya Kwanza: Misingi inayotumika kwa waandishi wa habari wa vyombo vya habari vya magazeti, redio, televisheni na vyombo vya habari vya mitandaoni; Sura ya Pili: Misingi inayotumika kwa waandishi wa vyombo vya habari vya utangazaji tu; Sura ya Tatu: Misingi inayotumika kwa waandishi wa habari mitandaoni tu na Sura ya Nne: Misingi inayotumika kwa wachapishaji na wamiliki wa vyombo vya habari.

# MAANA YA DHANA NA MANENO MUHIMU

**Wanahabari:** Watu wenye taaluma ya habari/vyombo vya habari wanaofanyakazi ya mawasiliano.

**Maslahi ya Umma:** Msemo huu unatumika katika muktadha wa aina mbalimbali. Maana yake hubadilika kutokana na muktadha. Kwa muktadha wa kanuni hizi, maslahi ya umma yana maana zifuatazo: Masuala yote yenye manufaa ya pamoja kwa umma, msingi kwamba jamii kwa ujumla wake ina maslahi na jambo husika; masuala yanayowaunganisha (wanajamii), kulinda na kuendeleza ustawi wa umma.

**Uandishi wa Hisia:** Ni ukuzaji wa tukio au mada kwenye habari, ikiwemo kutoa taarifa isiyojitosheleza na uwasilishaji habari wenye upendeleo kwa kujikita katika ushabiki na bila ya uwiano. Pia unahusisha kuandika habari zenye lengo na makusudi ya kuridhisha hisia za wapokeaji wa habari.

**Ushabiki:** Ni shauku kupita kiasi kuhusu jambo fulani. Hii ni pamoja na kufuata na kuamini jambo husika bila ya kuhoji.

**Ubaguzi:** Hii ni pamoja na ubaguzi wa watu au sifa, rangi, Taifa, jinsi, hadhi na kusababisha utofauti katika jamii.

**Kauli za chuki:** Ni kumshambulia mtu au kikundi kwa msingi wa rangi, dini, jinsi, mwonekano au Taifa zinazosababisha uwezekano wa kuchochea chuki, fujo, kutoelewana na ugomvi au ghasia. Halikadhalika kauli za chuki ni mawasiliano yenye lengo la kushusha hadhi, kuogofya au kuchochea ghasia/ugomvi au chuki dhidi ya mtu fulani kwa msingi wa rangi, kabila, Taifa, dini, jinsi au ulemavu wa aina yoyote.

**Tabia za Rushwa:** Ushawishi wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja au kampeni yenye lengo la kupata upendeleo kutoka kwa mtu mwenye wadhifa au ushawishi wa baadhi ya matokeo

**Mgongano wa maslahi:** Ni hali yenye uwezekano wa kudhoofisha uadilifu/ kuwa na upendeleo kwa mtu kutokana na uwezekanao wa mgongano wa maslahi yanayoendana (yanayowiana) na taaluma au ya umma. Kwa maneno mengine mgongano wa maslahi ni hali ambayo upande mmoja na upande wa pili unakwamisha utekelezaji wa wajibu wa upande wa tatu.

**Uhuru wa vyombo vya habari:** Ni uhuru wa kuripoti habari kinazopokea bila ya woga wowote wa kuadhibiwa. Pia unahusu vyombo vya habari visivyodhibitiwa na kundi lolote na vyenye uwezo wa kupata takwimu

muhimu.

**Uwajibikaji:** Ni kuwa na wajibu kamili wa matokeo yanayotokana na vitendo au shughuli anazofanya mtu au kuzichukua kwa hiari, kujitolea, kutumia akili kwa uangalifu mkubwa.

**Wajibu kwa jamii:** Ni majukumu yanayoekeleza vyombo vya habari kutilia mkazo mkubwa katika kuhimiza ustawi wa jamii kuliko maslahi ya kibiashara.

**Wizi wa maandishi:** Ni kitendo cha kutumia maandishi au mawazo ya mtu mwingine bila ya kutaja au kushukuru chanzo husika inavyotakiwa.

**Utashi:** Ni suala binafsi na hutofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine, sehemu ya jamii hadi nyingine na hivyo kuwa vigumu kwa watangazaji kuweka viwango vya utashi/matakwa vinavyokubalika kwa hadhara/walengwa.

**Staha:** Inahusu kuheshimu mila, asili, desturi za watu na imani zao. Dhana hii pia inachukuliwa tofauti kutegemeana na mtazamo wa mtu.

**Maudhui ya mtandaoni:** Ni maudhui yanayotayarishwa kupitia teknolojia mpya za mawasiliano (tofauti kabisa na magazeti, televisheni na redio). Hujumuisha intaneti, tovuti na vyombo vya habari mchanganyiko.

**Manufaa kwa jamii:** Ni kitendo kinachonufaisha idadi kubwa ya watu kwa kiwango kikubwa kadiri iwezekanavyo, kwa mfano maji safi, huduma za afya.

**Utu wa binadamu:** Ni haki ya mtu kuthaminiwa, kuheshimiwa na kutendewa kiuadilifu na kimaadili.

# SURA YA KWANZA

## MISINGI INAYOTUMIKA KWA WAANDISHI WA HABARI WA VYOMBO VYA HABARI VYA MAGAZETI, REDIO, TELEVISHENI NA VYOMBO VYA HABARI MTANDAONI.

### 1.0 Ukweli

Waandishi wa habari watasambaza habari na taarifa kwa misingi ya ukweli na haki kwa umma. Kwa matukio au masuala yanayohusu madai yenye utata au ubishani, yaonyeshe mfuatano wa ushahidi ukiwemo wa vyanzo vya binadamu na nyaraka. Aidha, ufanyike uhakiki wa kutumia chanzo zaidi ya kimoja. Habari itaonekana kuwa ni ya ukweli iwapo hoja za tukio au suala husika zinaeleweka kikamilifu na kuonyesha uhalisia wa tukio/jambo lenyewe kama ilivyoelezwa na pande zote zinazohusika katika suala la msingi.

### 2.0 Uhuru na mgongono wa maslahi

Waandishi wa habari watakuwa huru bila kuingiza maslahi yao au ushawishi kutoka nje, na wataripoti taarifa zao kwa kuzingatia hoja na ukweli bila ya woga wa kuadhibiwa au kushawishiwa na watu, vikundi vyenye maslahi kama vile watangazaji biashara, vyanzo, mada za habari, wamiliki wa vyombo vya habari, vikundi vingine vya ndani au nje. Waandishi wa habari pia watalinda na kutetea uhuru wao kutoka kwa wale wanaotaka kushawishi au kudhibiti maudhui ya habari. Uhuru utapatikana tu iwapo waandishi wa habari:

i) Wataamua kwa ukamilifu maudhui ya habari kwa kutumia uamuzi wa wahariri na sio matokeo ya ushawishi wa nje, ukiwemo wa wamiliki wa vyombo vya habari au menejimenti.

ii) Watazuia maslahi binafsi au shinikizo litakalodhoofisha uandishi wa habari na huduma kwa umma.

iii) Wataepuka mgongano wa maslahi pamoja na utaratibu au tabia zitakazoisababishia hadhira kuwa na shaka kuhusu

uhuru na weledi wa waandishi wa habari.

iv) Wataendelea kuwa huru bila ya kujihusisha na vyama pamoja na shughuli zitakazohatarisha uadilifu binafsi au kudhoofisha heshima ama sifa ya weledi wa vyombo vya habari.

## 3.0 Wajibu na uwajibikaji

Waandishi wa habari watambue wajibu wao kwa jamii na kuwa tayari kuupa kipaumbele ustawi wa jamii kwa maslahi ya gharama za shughuli zao na uhuru wa mtu mmojammoja. Ili kutimiza hayo:

i) Watazifanya habari kuwa ni kwa manufaa ya jamii na si bidhaa;

ii) Watawajibika kwao wenyewe, weledi wa taaluma na umma kwa ujumla ikiwemo maslahi ya jamii na si kwa wale wanaodhibiti au kumiliki vyombo vya habari.

## 4.0 Uaminifu na weledi wa vyombo vya habari

Waandishi wa habari watashiriki katika kuanzisha, kusimamia, kutekeleza na kufuata viwango vya juu vya mienendo ili kulinda uadilifu na weledi wa vyombo vya habari.

Ili kuhakikisha uaminifu na uadilifu wa weledi wa vyombo vya habari, kila mwandishi wa habari:

i) Atajitambulisha yeye na chombo cha habari anachofanya kazi. Matumizi ya mbinu za siri za kuweza kuingia katika maeneo yaliyodhibitiwa au kupata taarifa kutafanywa tu kwa maslahi ya umma na kwa idhini ya mhariri.

ii) Hatakiwi kumrekodi mtu bila mhusika kujua. Mwandishi anaweza kufanya kazi zake ikiwamo kurekodi iwapo ni muhimu ili kumlinda katika hatua ya kisheria au kwa sababu nyingine ya lazima.

## 5.0 Usahihi, uhakiki

Waandishi wa habari watahakikisha kuwa vyombo vyao vya habari vinalindwa wakati wote kwa usahihi na hawatapotosha kwa makusudi wasomaji kwa kuongeza au kuacha taarifa. Aidha, habari itakuwa sahihi na yenye uhakika iwapo:

i) Itakuwa na ukweli sio kwa muktadha sahihi kuhusu suala au mada husika tu, pia muktadha unaohusiana na habari hiyo na kuzihusilisha pande zote zinazohusika na suala au

mada husika.

ii) Maoni yaliyoelezwa kwenye habari hayapotoshi kwa kutoa msisitizo usiofaa au usio sahihi kwa kuhariri muktadha wa habari.

iii) Kwa tukio au suala linalohusu mada yenye utata, inawasilisha mfuatano wa ushahidi kama ulivyoelezwa na vyanzo pamoja na taarifa inayohusisha zaidi ya chanzo kimoja.

iv) Vichwa vya habari, vichwa vidogo na maelezo ya picha vinawasilishwa kwa usahihi na bila ya upendeleo, maudhui ya ripoti inayokusudia kueleza.

## 6.0 Haki na usawa

Waandishi wa habari watawatendea haki watu wanaohusika kwenye habari, kwa kuhakikisha kuwa wana fursa sawa ya kujibu lolote linalowahusu. Habari itaendelea tu bila ya majibu yanayohusika iwapo fursa ya kutoa maoni haina haja au iwapo mhariri amejiridhisha kwa ukamilifu kuwa hatua zote muhimu zimetumika. Habari itakuwa ya haki na usawa iwapo:

i) Itazipa pande zote za masuala ya msingi au mada, fursa ya kueleza upande wa pili wa habari yao au kutafuta na kuingiza maoni kutoka watu waoathiriwa au kuguswa.

ii) Inazipa haki sawa pande zote husika, upande mmoja unapotuhumu mwingine upate nafasi ya kujibu tuhuma hizo.

## 7.0 Haki ya kujibu

Waandishi wa habari watatoa fursa na haki ya kujibu waliohusika au taasisi/mashirika iliyoathiriwa au kuhusishwa kwenye habari kabla ya kuchapisha au kutangaza habari husika. Habari itaendelea tu bila ya majibu iwapo mhariri amejiridhisha kwa ukamilifu kuwa hatua zote muhimu zimezingatiwa.

Pale ambapo mhariri ana ushahidi wa kutosha kuwa hana shaka ya ukweli au usahihi na uhakika wa jibu au ufafanuzi atakuwa na uhuru wa kuongeza maelezo machache mwisho wa ufafanuzi kuonyesha msimamo wake kuhusiana na suala hilo.

## 8.0 Masahihisho

Waandishi wa habari na vyombo vyao vya habari watakuwa wazi kuhusu makosa. Kila itakapobainika kuwa habari haina usahihi,

inapotosha au yenye shaka imechapishwa au kutangazwa, itasahihishwa au kutolewa ufafanuzi haraka bila ya kusubiri kwanza malalamiko yatolewe.

Kwa lengo la usahihi, masahihisho yatafanywa kwa usahihi wa hoja na kutokana usahihi ufafanuzi utatolewa kwa taarifa inayopotosha au yenye shaka.

Masahihisho ni lazima yaeleweke na kuziomba radhi pande zote zinazohusika na yalingane na kosa kuhusu athari iliyotokea.

## 9.0 Habari za uongo

Ili kuepuka kueneza tetesi za uongo au kuendeleza kutoelewana ama kuwa chimbuko la taarifa zilizotungwa na za uongo kwa makusudi, kwa lengo la kudanganya na kupotosha wengine, waandishi wa habari wasijihusishe na:

i) Upotoshaji wa habari, kueleza taarifa ya uongo na iliyotayarishwa kwa makusudi kwa lengo la kumsababishia madhara mtu, kikundi cha jamii, shirika au nchi;

ii) Upotoshaji wa habari, kueleza taarifa ya uongo na iliyotayarishwa sio kwa lengo la kusababisha madhara.

iii) Habari inayofichua ukweli, kueleza taarifa inayohusu ukweli, inayotumika kuumiza mtu, kikundi cha jamii, shirika au nchi.

## 10.0 Dhana ya kutokuwa na hatia

Waandishi wa habari watafuata msingi wa dhana ya kutokuwa na hatia ambapo kila mlalamikiwa au mshitakiwa ataonekana hana hatia isipokuwa mpaka athibitike kuwa na hatia kwenye shauri lililo mbele ya mahakama.

## 11.0 Kupunguza madhara

Waandishi wa habari wasichapishe, kutangaza au kushirikishana taarifa na makala zitazohatarisha au kusababisha madhara makubwa kwa hadhira au wale wanaohusika na maudhui husika. Iwapo maudhui yanaweza kusambazwa, ni lazima juhudi zifanywe kuhakikisha kuwa chanzo cha maudhui kinaelewa hatari zitakazojitokeza na kutoa ridhaa kabla, na hatua za kupunguza hatari hiyo ziwepo.

## 12.0 Vyanzo vya habari visivyokuwa na jina

Waandishi wa habari na vyombo vyao vya habari waepuke kabisa kutumia vyanzo visivyokuwa na jina isipokuwa kama hakuna namna nyingine ya kushughulikia makala au habari husika. Kunahitajika umakini zaidi kuhakiki taarifa kutoka kwa vyanzo vya aina hiyo.

Taarifa itakayotoa siri isichapishwe au kutangazwa isipokuwa kwa maslahi ya umma.

## 13.0 Kutotangaza vyanzo vya habari

Mwandishi wa habari atalinda siri ya chanzo chake cha habari na atatoa hadharani kwa matakwa ya mahakama.

i) Watafuata kanuni za ndani za vyombo vyao vya habari na kupata ridhaa ya mhariri kabla ya kupewa siri. Baada ya kupewa siri hiyo, mwandishi wa habari na chombo chake wataiheshimu.

ii) Mhariri kwa kuwa ndiye mwenye mamlaka ya mwisho ya uhariri, atakuwa na hiari ya kutaka chanzo cha habari kwa mwandishi kwa sharti la kutoeleza chanzo hicho kwa mtu wa tatu.

## 14.0 Ukweli na maoni

Waandishi wa habari watatofautisha wazi kwenye ripoti zao baina ya maoni, dhana na ukweli. Habari zitabaki kutopendelea ingawa mwandishi wa habari anaweza kuwa shabiki katika makala za maoni na matukio.

## 15.0 Kurekodi mahojiano na mazungumzo kwa njia ya simu

Isipokuwa kwa ajili ya kuthibitisha tu, waandishi wa habari hawatarekodi au kunasa sauti ya mtu bila ya mhusika kujua. Hata hivyo, mwandishi anaweza kufanya kazi zake ikiwamo kurekodi iwapo ni muhimu ili kumlinda katika hatua ya kisheria au kwa sababu nyingine ya lazima.

## 16.0 Kuheshimu faragha na utu wa mtu

Waandishi wa habari wanatakiwa kuelewa mipaka ya maeneo ya umma na binafsi. Kwa muktadha huu:

i) Uingiliaji na uvamizi wa maisha binafsi na faragha bila ridhaa

ya mtu anayehusika hakutakubalika, isipokuwa kama maslahi ya umma yatazidi haki za faragha.

ii) Mambo yanayohusu nyumba binafsi, familia, dini, kabila, jinsi, maisha binafsi na mambo ya faragha ya mtu binafsi ni lazima yachukuliwe kwa dhana ya faragha, isipokuwa pale yanapoathiri umma.

iii) Uchapishaji wa taarifa kuhusu watu binafsi utakubaliwa iwapo taarifa hiyo ni kwa ajili ya kuchunguza au kuelezea mwenendo wa uhalifu, kuchunguza au kuelezea mwenendo mbaya wa matukio yasiyokuwa ya kiungwana; kulinda afya na usalama wa umma; na kuzuia umma usipotoshwe na matamko au vitendo vya mtu husika ambapo mtu mwenyewe anafanya jambo kwa faragha na kulaani hadharani.

## 17.0 Uingiliaji wakati wa majonzi na mshituko

Katika kushughulikia masuala ya kijamii ya hali ya kushtua au hisia kali kama vile ukatili, kutumia nguvu, matumizi ya dawa za kulevya, ufuska, maneno machafu, waandishi wa habari watawasilisha ukweli, maoni, picha na michoro kwa uangalifu mkubwa na busara. Utekelezaji utafanywa kwa uangalifu na busara. Kwa hali hiyo, waandishi wa habari:

i) Watajitambulisha na kupata idhini ya kuhoji kutoka kwa mtendaji anayehusika kabla ya kuingia katika maeneo yasiyokuwa ya wazi ya hospitali au taasisi nyingine.

ii) Wataepuka kutumia habari, picha na kutumia tena picha za maktaba za matukio ya kifo na maradhi ya hatari ya watu, kufufua majonzi miongoni mwa ndugu, jamaa na marafiki. Hali kadhalika, watatumia taarifa kwa busara kuhusu marehemu na sababu za kifo.

iii) Wasijinufaishe kwa utumiaji wa makusudi wa matukio ya walioathiriwa na majonzi.

## 18.0 Kuripoti migogoro ya kikabila na kidini

Waandishi wa habari wasichapishe, kusambaza au kutangaza habari, maoni au mtazamo kuhusu migogoro ya kikabila na kidini kabla ya kuhakiki usahihi na ukweli wa taarifa. Taarifa ya aina hiyo iwasilishwe kwa tahadhari kubwa na kuzuia migogoro. Aidha, iwasilishwe kwa namna inayofaa kujenga na kuleta hali

ya urafiki na utulivu kwa taifa, kujenga uhusiano mwema wa amani na sio katika hali itakayoweza kuchochea hisia kali, kuzidisha mvutano au kuongeza uhasama baina ya jamii au pande zinazohusika.

## 19.0 Sifa na utu

Vyombo vya habari vitakuwa makini na kuzingatia mambo yanayohusu sifa na utu wa watu wengine. Katika kulinda faragha, sifa na utu ni lazima kutia uzito maalumu katika mila na desturi kuhusu faragha na utu wa waathiriwa wa makosa ya ngono, watu ambao wakiwa ni watoto na wazee pamoja na watu wenye ulemavu wa viungo na akili. Utu wa mtu utapuuzwa tu iwapo ni kwa maslahi ya umma na katika mazingira yafuatayo:

i) Utoaji taarifa mahali pa tukio utakuwa wenye maoni ya haki kwa msingi wa ukweli unaoonekana vya kutosha na kwamba ni sahihi.

ii) Utoaji taarifa mahali pa tukio utakuwa wa haki na ripoti sahihi ya mwenendo wa mashtaka mahakamani, majadiliano bungeni au kwenye mabaraza mengine yenye hadhi ya kimahakama au mikutano.

iii) Ilikuwa sahihi kwa taarifa kutolewa kwa sababu ilitayarishwa kwa kuzingatia misingi ya mwenendo wa kiuandishi habari inayokubalika na kwa maslahi ya umma.

## 20.0 Uzingatiaji jinsia

Waandishi wa habari waepuke kutumia maneno na kauli zinazoonyesha kuwa jinsia moja ni duni kuliko nyingine au kuendeleza ubaguzi wa kijinsia au kukosa usawa. Ni lazima wahakikishe wanawatendea kwa usawa wanaume na wanawake wakati wa kuchagua chanzo cha habari na kuacha utoaji wa taarifa unaochochea chuki au kushawishi vurugu kwa msingi wa jinsia.

## 21.0 Utoaji habari za watu wenye ulemavu na makundi yaliyo katika mazingira magumu

Waandishi wa habari wasichapishe, kutangaza au kushirikishana taarifa zinazokusudia kuzihaki au kudharau watu kwa misingi ya jinsia zao au ulemavu wa viungo. Halikadhalika, waepuke kutumia maneno au misemo, mabango au picha zinazozihaki au kuonyesha chuki dhidi ya watu kutokana na hali zao.

## 22.0 Maneno machafu, utashi na jinsi ya utoaji taarifa

Waandishi wa habari wasichapishe taarifa zenye maneno makali isipokuwa machapisho hayo ni kwa maslahi ya umma. Hata hivyo, tahadhari zifuatazo lazima zichukuliwe:

i) Picha zinazoonyesha miili iliyokatwakatwa, matukio ya umwagaji damu, matukio ya kuchukiza ziepukwe.

ii) Pale ambapo picha za namna hiyo haziwezi kuepukika, zisilenge viungo vya siri/vya uzazi au sehemu zinazowadhalilisha watu na marekebisho makubwa ikiwemo ukataji, upunguzaji ukubwa, marekebisho ya rangi ndivyo vitakavyoruhusiwa.

iii) Tahadhari itatolewa kuwaonya watazamaji au wasomaji wa taarifa inayochapishwa au kutangazwa.

Waandishi wa habari wasichapishe, kutangaza wala kushirikishana maudhui ya habari yasiyovutia na yasiyo na staha, heshima au maadili. Sheria, kanuni na viwango kuhusu heshima vilivyowekwa na mamlaka zinazosimamia vyombo vya habari vitatumika kuwaelekeza waandishi maudhui yanayostahili.

## 23.0 Matumizi ya picha na majina

Waandishi wa habari wanatakiwa kuchukua tahadhari katika kutumia picha na majina na waepuke kuchapisha taarifa kunapokuwa na uwezekano wa kuwaathiri watu wanaohusika. Katika muktadha huu:

i) Kutumia picha kwa lengo la kupotosha ukweli na usahihi wa habari kuepukwe.

ii) Picha/video au maudhui ya sauti yasipotoshe au kutowakilishwa kwa usahihi, picha/video au maudhui ya sauti yasichezewe kutimiza manufaa hayo. Maelezo chini ya picha yatafafanua kwa usahihi maudhui ya picha au picha zinazohusika.

iii) Picha za majonzi, maafa na zile zinazoaibisha na kuhamasisha ubaguzi wa kijinsia zisitumike.

## 24.0 Kuwalinda Watoto

Maslahi ya watoto ni muhimu sana katika kila jambo linalohusu mtoto. Hivyo, waandishi wa habari wanatakiwa:

i) Kuepuke utoaji wa taarifa zitakazosababisha madhara ya aina yoyote kwa mtoto, isipokuwa kama usambazaji wa aina hiyo ndiyo njia pekee ya kushughulikia maslahi ya mtoto.

ii) Wasiwahoji, kuwapiga picha au kuwabainisha watoto bila ya ridhaa ya mlezi halali kisheria au mtu mzima mwenye dhamana.

iii) Wasichapishe au kutangaza majina ya wahalifu wenye umri mdogo (chini ya miaka 18) waliokamatwa na polisi au kuhukumiwa kwenye mahakama za jinai. Iwapo ubainishaji huo ni lazima ufanywe, chombo cha habari kitaeleza sababu za msingi za wahariri kufanya uamuzi huo.

iv) Wasiwabainishe watoto walionyanyaswa, kutumika vibaya, au walioshitakiwa au kupatikana na hatia ya jinai.

v) Wasiwabainishe watoto waliohusika katika kesi au mashauri yanayohusu makosa ya kingono, kama waathiriwa, mashahidi au washitakiwa.

## 25.0 Ubaguzi na kauli za chuki

Waandishi wa habari waepuke kuonyesha ubaguzi au kupaka matope watu kutokana na ukabila, jinsi, ujauzito, ndoa, asili ya jamii au kabila, rangi, historia, umri, ulemavu, dini, dhamira, imani, utamaduni, lugha na uzawa, hali ya maambukizo ya UKIMWI au hali nyingine wala wasitaje hali ya mtu katika muktadha wa kashfa au chuki isipokuwa pale ambapo ni lazima kwa jambo hilo kuripotiwa na kwa maslahi mapana ya umma.

## 26.0 Vurugu na maudhui ya michoro

Umakini na uwajibikaji wa kutosha utafanywa na vyombo vya habari kuhusu uwasilishaji wa taarifa za ukatili, vurugu isiyo ya lazima na mateso. Kutokana na hali hiyo wafanyakazi wa vyombo vya habari:

i) Watashughulikia kwa tahadhari habari zinazochochea vurugu au tabia chafu au ubaguzi kwa msingi wa jinsia, kabila, rangi, asili, dini, imani au hali ya kijamii na kiuchumi.

ii) Waepuke, maudhui yanayoonyesha uhalifu unaotumia nguvu au vurugu nyingine au tabia dhahiri za ngono isipokuwa kama maslahi ya umma yatataka hivyo.

iii) Wataonyesha “onyo” kabla ya kuonyesha maudhui au

michoro isiyofaa kwa baadhi ya watu kama vile watoto.

## 27.0 Ndugu na marafiki wasio na hatia

Waandishi wa habari wasiwabainishe ndugu au marafiki wa watu wenye hatia au walioshitakiwa kwa uhalifu isipokuwa kama kuonyeshwa kwao ni muhimu kuripoti kwa ukamilifu, kwa haki na kwa usahihi mashauri ya uhalifu au kisheria.

## 28.0 Uchochezi wa ugomvi

Waandishi wa habari wasichapishe au kutangaza habari inayokusudiwa au kukaribia kusababisha uadui au chuki kwa watu, kwa msingi wa kikabila, kijamii, kidini, kitaifa au chama cha siasa. Watachukua tahadhari zaidi kuepuka kuchangia au kueneza chuki wakati wanaporipoti matukio ya aina hiyo.

## 29.0 Vitendo vya rushwa

Waandishi wa habari wasiombe, kushawishi, kupokea hongo, zawadi au manufaa mengine yanayokusudiwa kushawishi uamuzi wa taaluma ya habari.

*i)* ***Zawadi na ukarimu***

Wakatae tunzo, burudani, zawadi au upendeleo binafsi ambavyo kwa namna yoyote ile vitashawishi au kuonyesha kushawishi uamuzi wao wa taaluma ya habari. Katika hali ambapo zawadi zinatolewa, mpokeaji ni lazima aeleze mamlaka ya ofisi yake kupokea kwake zawadi au takrima.

*ii)* ***Kupewa upendeleo au fadhila***

Wasikubali kupokea upendeleo wowote ili kuepuka hali ambayo watakuwa katika jukumu la kurudisha fadhila. Halikadhalika, wasitumie nyadhifa zao au maarifa waliyopata kutokana na matokeo ya nyadhifa zao kwa manufaa yao binafsi au ya faragha.

*iii)* ***Malipo ya taarifa au vyanzo***

Waandishi wa habari wasitoe fedha au zawadi kwa lengo la kushawishi vyanzo vya habari kutoa taarifa baada ya kuwapa fedha ambazo ni sawa na kununua habari na kufanya habari kuwa aina fulani ya bidhaa ya biashara ambayo haitakiwi kuwa hivyo.

iv) ***Malipo ya kuchapisha au kutangaza habari***

Waandishi wa habari wasipokee fedha au aina yoyote ya malipo kama motisha ya kuchapisha taarifa. Halikadhalika wasichapishe, kutangaza au kuzuia taarifa au kubadilisha baadhi ya taarifa muhimu kwenye ripoti kutokana na kulipwa fedha au zawadi au tunzo yoyote.

## 30.0 Wizi wa maandishi

Waandishi wa habari wajiepushe na wizi wa mawazo au maandishi ya watu. Kutokana na hayo:

i) Wataje moja kwa amoja chanzo cha habari walichonukuu zaidi ya utoaji wa taarifa ya mwandishi mwenyewe,

ii) Wahakikishe kuwa maudhui yaliyochapishwa au kutangazwa katika habari au vipindi hayana wizi wa kimaandishi au mawazo ya mtu na taarifa yoyote yenye maudhui yaliyoazimwa itaje chanzo kwa haki ya mwandishi wa awali.

## 31.0 Matangazo.

Vyombo vya habari visiruhusu tangazo lolote kinyume na kipengele chochote cha maadili haya ya waandishi wa habari.

## 32.0 Utaratibu wa kupata maoni

Wachapishaji au vituo vya utangazaji viweke utaratibu wa kupata maoni unaoeleweka kwa madhumuni ya kushughulikia madai au malalamiko yanayotolewa na wasomaji au wasikilizaji/ watazamaji.

# SURA YA PILI

## MISINGI INAYOTUMIKA KWA WAANDISHI WA HABARI WA VYOMBO VYA HABARI VYA UTANGAZAJI TU

### 1.0. Mahojiano

Mahojiano ni njia maarufu sana katika utangazaji wa hoja za mtu husika. Hata hivyo, ni lazima kuwa makini kwa kuzingatia misingi ya haki, kutopendelea, uadilifu, busara na uwiano wa kupata maoni ya aina tofauti. Kwa muktadha huu watangazaji:

i) Wasifanye mazoezi ya majadiliano au kuwasilisha maswali mahususi kabla. Inaruhusiwa kujadiliana mapema na mhojiwa, madhumuni ya mahojiano na mada za jumla zikazoshugulikiwa.

ii) Wapange, waendeshe na kuhariri mahojiano, uchambuzi, vikao na majadiliano katika redio na televisheni bila ya upendeleo.

iii) Wasiharibu wala kupotosha maoni ya washiriki au kutoa maoni tofauti.

iv) Wasiwasilishe maelezo waliyorekodi kabla kama mahojiano mbashara, uchambuzi na majadiliano.

v) Wawape wanaopiga simu tahadhari ya mapema kuhusu kurekodi simu zinazoingia ili kuepuka matumizi ya lugha ya kushambulia na ubaguzi wa rangi na kijinsia.

### 2.0. Vipindi mbashara vya kupiga simu

Vipindi mbashara vya kupiga simu ni njia ya utoaji mawazo, maoni na mtazamo wa mtu mmojammoja inayokubalika na maarufu. Hata hivyo, kunahitajika uangalifu ili kudumisha misingi ya haki bila ya upendeleo, uadilifu, busara katika uwiano wa kupata maoni, mawazo na mitazamo ya aina mbalimbali. Kwa muktadha huu, watangazaji wa vipindi mbashara vya kupiga simu:

i) Waendeshe majadiliano kwa kuwianisha mawazo na siyo

kama chombo cha kutoa maoni binafsi hewani na lazima wawatendee haki wapiga simu wote bila ya upendeleo.

ii) Walinde vipindi dhidi ya kutekwa na vikundi vya wanaharakati au watu wasiowajibika.

## 3.0. Njia ya udhibiti na nidhamu

Vipindi vinavyotangazwa vikiwemo vya mazungumzo na majadiliano vitadumisha utulivu na kuonyesha weledi wa kitaaluma pamoja na mfano wa mazungumzo ya kistaarabu, busara na yanayoheshimu haki za binadamu. Kwa mantiki hiyo waendeshaji wa vipindi wahakikishe kuwa:

i) Vipindi havina mada zitazokuwa na mwelekeo wa kuchochea vurugu na ugomvi.

ii) Kuzungumzia vurugu na mivutano ni lazima iwianishwe na iwe ya kweli.

## 4.0. Upangiliaji

Watangazaji wana jukumu la kupanga vipindi vyenye maudhui yasiyoonyesha watoto na watoto wadogo katika matukio ya vurugu na mashambulizi. Kwa hali hiyo ni lazima wazingatie kuwa:

i) Vipindi vinavyotangazwa wakati wa vurugu visirudiwe baada ya matukio hayo.

ii) Maudhui yanayoonyesha au yenye matukio ya vurugu au ugomvi, lugha ya chuki au yanayowalenga watu wazima yasitangazwe nje ya wakati husika.

iii) Lugha kali ya chuki isitumike kwenye maudhui ya vipindi vinavyotangazwa nje ya wakati wa vurugu au wakati ambao idadi kubwa ya watoto huenda wakawa sehemu ya watazamaji.

## 5.0. Vipindi vya watoto

Watangazaji wana jukumu la kuwalinda watoto dhidi ya vipindi au maudhui yenye madhara au visivyopendeza kwa watoto. Ili kutimiza hayo, watangazaji ni lazima wazingatie yafuatayo:

i) Wasitangaze taarifa yenye madhara au kuwatia wasiwasi watoto katika nyakati ambazo idadi kubwa ya watoto huenda wakawa sehemu ya watazamaji.

ii) Katika vipindi vinavyoonyesha wahusika kuhusu maisha halisi, matukio ya vurugu ama uhalisia wa maneno au hisia/ mihemko vionyeshwe iwapo ni lazima kufanya hivyo kwa ajili ya kumjenga mhusika kupitia kisa husika.

iii) Vipindi vya katuni kwa watoto ambavyo vinakubalika kuwa ni mtindo wa kusimulia hadithi vinaweza kuwa na ugomvi wa kuigiza tu na sio kweli, visiwe na ugomvi kama msingi mkuu na visichochee katuni za hatari.

iv) Vipindi vya watoto vishughulikiwe kwa umakini zaidi, dhamira zinazotishia hisia za usalama wao wakati vinapoonyeshwa, kwa mfano ugomvi wa nyumbani, kifo, uhalifu au matumizi ya dawa za kulevya au ulevi viepukwe.

v) Vipindi vya watoto vishughulikie kwa umakini dhamira zinazoshawishi watoto waige vitendo wanavyoviona kwenye televisheni au wanavyovisikia kama vile matumizi ya mifuko ya plastiki kama vitu vya kuchezea, matumizi ya vibiriti au vyombo vya nyumbani vya hatari kama vitu vya kuchezea.

vi) Vipindi vya watoto visiwe na matukio halisi ya ugomvi yatakayoleta hisia kwamba ugomvi ndiyo njia inayotakiwa au ya pekee ya kutanzua ugomvi baina yao.

vii) Vipindi vya watoto visiwe na matukio halisi ya ugomvi yanayochochea au kuficha athari za vitendo vya ugomvi na kutumia nguvu. Uonyeshaji wowote wa hali halisi ya ugomvi ni lazima uonyeshe athari au matokeo ya ugomvi kwa binadamu wakiwemo waathirika na walioanzisha ugomvi.

## 6.0. Usalama

Watangazaji wana wajibu wa kuhakikisha kuwa hawatangazi vipindi au maudhui yanayoweza kuhatarisha usalama wa watoto. Katika kuhakikisha hilo:

i) Wasitangaze kipindi chochote kwa mdomo au michoro kwa watoto kushiriki katika vitendo visivyo salama au hali isiyo salama au maudhui yanayowahimiza waingie mahali pa ajabu au kwenye hatari isipokuwa kama pametangazwa maalumu kwa ajili ya usalama.

ii) Wasitangaze vitu vinavyotumiwa katika hali ya hatari au isiyo salama ama visivyokuwa salama iwapo vitatumiwa na watoto bila ya usimamizi, isipokuwa kama imetangazwa

maalumu kwa ajili ya usalama.

iii) Wasionyeshe vitu vyenye uhalisia kama silaha na kuvifananisha na silaha halisi.

iv) Wahifadhi vipindi vyenye matangazo kwa angalau miezi mitatu, endapo kutakuwa na malalamiko kutoka kwa wasikilizaji au watazamaji.

## 7.0. Tahadhari kwa maudhui yasiyopendeza, yanayochukiza na yenye mashambulizi

Watatangaza tahadhari kabla au wakati wa kuanza programu yoyote yenye lugha au picha zinazoweza kukirihisha au yenye mashambulizi kwa watazamaji wa kawaida au wasikilizaji kwa kuzingatia muda na nafasi.

## 8.0. Uhariri na viwango vya utayarishaji

Watu wote wanaohariri ripoti, mahojiano na taarifa kwa ajili ya kutangazwa wahakikishe kuwa uhariri wao unaonyesha kwa haki bila ya upendeleo uaminifu na bila ya upotoshaji wa kilichoonekana na kusikika. Kwa hali hiyo yafuatayo yazingatiwe:

i) Mahojiano yahaririwe vizuri, kuhifadhiwa hata kama ni sehemu fupi za sauti ili kulinda maana halisi ya mahojiano.

ii) Majibu yasitolewe kwenye muktadha au kuhaririwa katika hali itakayobadili maana. Maelezo yatakayoongoza kwenye sehemu ya sauti yaonyeshe swali lililosababisha jibu.

## 9.0. Masuala ya utata yenye umuhimu kwa umma

Wakati wa kuwasilisha kipindi chenye masuala tata yenye umuhimu kwa umma yajadiliwe. Yafuatayo yazingatiwe:

i) Mtangazaji afanye juhudi za kutosha kuwasilisha hoja za mawazo zinazokinzana katika ama kipindi hicho au kipindi cha baadaye ambacho ni sehemu ya mfululizo wa kipindi husika vinavyotangazwa kwa muda na wakati uleule.

ii) Mtu ambaye maoni yake yatakosolewa kwenye kipindi kinachotangazwa kuhusu suala la utata lenye umuhimu kwa umma, apewe haki ya kujibu kwenye kipindi hicho hicho.

## 10.0. Vibonzo

Vipindi vya televisheni visiingize ugomvi mkubwa au matukio

ya mateso kwenye katuni au vibonzo vinavyoonyesha wahusika, wala visionyeshe katuni au vibonzo vinavyoshambulia watu kwa msingi wa kabila, dini au jinsi yao.

## 11.0. Uchaguzi na kura ya maoni

Wakati wa uchaguzi wowote au kipindi cha kura ya maoni kama ilivyoelezwa katika sheria na kanuni za uchaguzi husika kila baada ya muda, watangazaji wote wafuate masharti yaliyoelezwa na mamlaka zinazosimamia uchaguzi au kura ya maoni.

## 12.0. Ushindani kwa ajili ya usawa

Watangazaji wahakikishe kuwa vipindi na promosheni zote zinazotoa zawadi au tunzo havina njama baina yao na washindani wao ili kuepuka upendeleo usio wa haki baina ya mshindani mmoja na mwingine.

## 13.0. Matangazo ya biashara

Wakati wa kutangaza matangazo ya biashara, watangazaji watekeleze wajibu wao kwa mujibu wa kanuni za taaluma na weledi wa uandishi wa habari, pamoja na sheria na kanuni nyingine (Kanuni za TCRA). Kwa hali hiyo:

i) Waache kushiriki katika shughuli haramu na kujiingiza katika mambo yasiyozingatia weledi wa kazi.

ii) Wahakikishe kuwa muda wa matangazo ya biashara hauzidi asilimia 30 ya jumla ya muda wa matangazo ya vipind kwa siku.

iii) Wasiwapotoshe wasikilizaji/watazamaji kwa utata au athari za sauti na picha.

iv) Wasitumie ulinganishaji wa bidhaa katika matangazo ya biashara bila ya upendeleo, kwa misingi ya ukweli unaoweza kuthibitishwa.

v) Wasitumie kwa vyovyote vile matangazo ya biashara yanayoashiria dharau au kuumbua washindani au bidhaa.

vi) Watoe ushuhuda wa kweli na wahusishe na uzoefu binafsi wa mwidhinishaji. Ushuhuda na idhini inayotolewa na mtoto isitumiwe.

## 14.0. Uhakikisho na zawadi

i) Wawe makini zaidi kwa matangazo yanayotoa uhakikisho. Kuhakikisha kuwa huduma iliyoahidiwa inapatikana kama ilivyoelezwa.

ii) Waepuke kutangaza huduma na bidhaa za bure mpaka ziwe zinapatikana bila ya gharama yoyote au gharama za ziada, isipokuwa za posta na usafirishaji.

iii) Wahakikishe kuwa wanamtambulisha mteja mwenye tangazo linalohusu jambo la umma au kisiasa ama kampeni kwa sauti au picha.

iv) Watangazaji kwa vyovyote vile kamwe wasitoe kamisheni, punguzo au motisha nyingine kwa watu au vikundi vinavyojihusisha na mwenendo usio wa kiuadilifu.

## 15.0. Kilevi, tumbaku, usalama wa barabarani na masuala ya mazingira

Zingatia maadili ya ndani ya nchi ya mashirika ya utangazaji yanayohusika kabla ya kukubali au kutangaza matangazo ya biashara yanayohusika na bidhaa zenye uwezekano wa kuathiri afya, usalama na kuleta madhara kwa mazingira.

## 16.0. Uwasilishaji

Katika utangazaji baadhi ya bidhaa zinazotangazwa zinaeleza kuwa wazi katika uunganishaji au vitu vya ziada kama vile (maandishi katika betri au mavazi), vinahitajika kabla ya bidhaa hizo kutumika ili zilete matokeo yaliyotangazwa.

Wasipuuze kiwango cha stadi zinazotakiwa na mtoto kutumia bidhaa. Stadi inayotakiwa kupata matokeo yaliyoonyeshwa lazima ipatikane kwa mtoto wa kawaida katika rika ambalo bidhaa hiyo inatangazwa.

## 17.0. Mashindano

Katika utangazaji wa maudhui yanayohusu mashindano, eleza wazi kanuni na masharti ya mashindano husika. Thamani ya zawadi na uwezekano wa kushinda visikuzwe au kusifiwa sana.

## 18.0. Udhamini

i) Wakubali udhamini kutoka kwa mashirika yanayokubalika

kisheria na jamii.

ii) Waepuke kutangaza matangazo yanayodhoofisha afya na ustawi wa jamii.

iii) Waepuke kutangaza matangazo yanayohatarisha weledi au kuathiri ubora na uadilifu wa chombo cha habari kinachohusika.

iv) Watangazaji watofautishe baina ya taarifa iliyotangazwa kutoka kwa wafadhili, maudhui yaliyolipiwa na maudhui ya habari.

## 19.0. Uchambuzi, maelezo na tahariri

Matangazo yote ni lazima yawe na taarifa ya usuli ya kutosha na maelezo kuwezesha hadhira kuelewa vizuri umuhimu na matokeo ya taarifa inayoripotiwa. Waandishi wa habari wasiingize maoni yao binafsi au hukumu kwenye ripoti zenye ukweli wakati wowote.

i) Vipindi vinavyohusu masuala nyeti ya umma, misingi ya taifa, mambo ya umma na maelezo vishughulikiwe na watu wenye maarifa ya kutosha tu na wanaozingatia maadili ya utangazaji. Kwa upande mwingine, wazungumzaji waalikwa kwenye vipindi ni lazima wawe watu wenye weledi na sifa katika mambo yanayozungumzwa.

ii) Vipindi vya masuala ya umma vinavyotangazwa katika muda uliolipiwa na watu wengine, vitaje jina la mwenye jukumu la kutayarisha vipindi wakati wowote vinapotangazwa.

iii) Pande zinazokinzana au kutofautiana kuhusu masuala ya umma ni lazima zipewe haki bila upendeleo.

iv) Upendeleo binafsi au chuki visiruhusiwe kupotosha ukweli.

## 20.0. Maudhui yaliyoandaliwa kwa mtumiaji kutangazwa kwenye televisheni au redio

Katika hali ambayo maoni yamechukuliwa kutoka kwa hadhira kwa madhumuni ya kuongeza mwelekeo wa maudhui yaliyoletwa, wahariri au watayarishaji wazingatie hatua zifuatazo za udhibiti:

i) Kutumia na kuchapisha wazi na kwa umuhimu kwenye tovuti zao sera za usimamizi wa maudhui ya watu wengine, na sheria ambazo watumiaji lazima wazifuate kuongeza

maoni au maudhui kwenye kurasa zao. Sheria hizi zieleze wazi maudhui ya watu wengine yanayoruhusiwa watangazaji kutangaza, ushughulikiaji wa maoni yasiyo na jina la mtoaji na taratibu za malalamiko au taarifa za ukiukaji wa sera au sheria za tovuti.

ii) Kufuatilia tovuti zao na kurasa za mitandao ya kijamii inayohusika na kuchukua hatua za kuzuia au kusitisha utangazaji wa maudhui yasiyo halali au yanayokiuka misingi na hadhi ya utu, faragha na yenye kauli ya chuki. Pale inapowezekana ufuatiliaji huo ufanywe kabla ya uchapishaji au utangazaji.

iii) Kuwapo kwa sera za usimamizi wa maudhui zinazoonyesha aina ya ufuatiliaji wa maudhui yanayotokana na utumiaji ambazo tovuti zinatumia (Kabla na baada n.k) na teknolojia gani zinatumika kwa madhumuni haya.

iv) Kutumia kadri inavyowezekana mbinu za udhibiti zilizopo au teknolojia nyingine ili kuzuia uchapishaji wa lugha ya fedheha au matusi ama maudhui mengine yanayoweza kutambuliwa kwa urahisi na yasiyofaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa maudhui yanayotangazwa kwenye televisheni au redio ni salama.

v) Kuchukua hatua ya haraka kuchunguza na kuondoa maudhui yasiyokubalika mara tu wahariri au watayarishaji watakapobaini. Wachukue hatua kwa ridhaa yao (hata kama hakuna malalamiko yaliyotolewa na watu walioathiriwa au watu wengine) na kushughulikia haraka baada ya kupata malalamiko halali.

vi) Wawe na sera na taratibu maalumu za kutambua na kuondoa haraka maudhui ya ngono au picha za siri zisizokubalika (picha, video, n.k) kutokana na faragha au usiri na kulinda heshima na utu wa mtu.

## 21.0. Matumizi ya maudhui ya wengine kutoka kwenye mitandao au yaliyotolewa na umma

Picha binafsi, video au taarifa zilizoandikwa na kuchapishwa kwenye mitandao ya kijamii, zinahesabiwa kuwa ni mali au milki ya umma na kutumiwa katika vyombo vya mawasiliano. Kutokana na hali hiyo watangazaji:

i) Wazingatie athari ya kutumia taarifa hizo za mtu binafsi, hasa kuhusiana na matukio ya kusikitisha kama vile misiba. Pia suala la hakimiliki lizingatiwe.

ii) Picha na video wanazochukua kutoka kwenye mitandao ya kijamii wazichambue kwa umakini na wazihakiki kujua uhalisia wake.

iii) Uwezo wa kupata picha au video kutoka kwenye mitandao ya kijamii au kurasa binafsi hakuzuii vyombo vya habari kutimiza jukumu lao la kuchukua tahadhari. Maslahi ya umma katika kuchapisha taarifa hizo lazima yapimwe dhidi ya haki binafsi na kuwalinda watoto. Uchapishaji wa picha kwenye mitandao ya kijamii usichukuliwe kuwa ni ridhaa ya chanzo asili kuchapisha tena kwenye maeneo mengine kama vile kwenye vyombo vya mawasiliano na umma.

## 22.0. Matukio ya jukwaani

Wapiga picha na watayarishaji video waonyeshe matukio ya jukwani wanapochukua video au mada za picha katika studio, waepuke kuwapotosha watazamaji kuamini kuwa hali hiyo imepatikana wakati wa kukusanya habari. Hatua zozote ni lazima zielezwe ili wasijeona kuwa ni juhudi za kudanganya.

# SURA YA TATU

## MISINGI INAYOTUMIKA KWA WATAYARISHAJI WA MAUDHUI YA MITANDAONI

### 1.0. Maudhui kutoka kwa mtumiaji

i) Wahariri au watayarishaji wa maudhui ya mtandaoni wafuatilie tovuti zao na kurasa za mitandao ya kijamii, na kuchukua hatua kuzuia au kusitisha uchapishaji wa maudhui yasiyozingatia uadilifu na yanayokiuka utu wa mtu au faragha, ama kusababisha kauli ya chuki. Pale inapowezekana ufuatiliaji huo ni lazima uwe kabla ya uchapishaji.

ii) Wahariri na watayarishaji wa maudhui ya mtandaoni watumie na kuchapisha wazi kwenye tovuti zao sera zao za usimamizi wa maudhui kwa mtu mwingine, na sheria ambazo watumiaji lazima wafuate kuongeza maoni au maudhui mengine kwenye kurasa zao. Sheria hizi zieleze waziwazi maudhui ya mtu mwingine yanayoruhusiwa, ushughulikiaji wa maoni yasiyokuwa na jina na taratibu za taarifa za ukiukaji wa sera na sheria za tovuti.

iii) Sera za usimamizi wa maudhui zionyeshe waziwazi aina gani ya maudhui yaliyotoka kwa mtumiaji zinatumiwa na tovuti (kabla, baada n.k) na teknolojia zinazotumiwa kwa madhumuni hayo. Wahariri au watayarishaji wa maudhui mtandaoni watumie kadri iwezekanavyo vidhibiti vilivyopo au teknolojia nyingine kuzuia uchapishaji wa lugha ya matusi au maudhui mengine yasiyofaa.

iv) Wahariri au watayarishaji wa maudhui mtandaoni wawapatie watumiaji utaratibu rahisi wa kuripoti maudhui ya mtu wa tatu ambayo wanaona hayana maadili au yanakiuka sera za tovuti.

v) Kuhusu maoni yanayoonyesha kauli ya chuki, yanayohatarisha usalama au uadilifu wa mtu mmojammoja au yanayoweza kusababisha ukiukaji wa haki za binadamu, wahariri na watayarishaji wa maudhui ya mtandaoni watumie taratibu zinazofaa kubainisha na kuondoa au kuzuia maudhui hayo haraka iwezekanavyo.

vi) Wahariri na watayarishaji wa maudhui mtandaoni waanze kuchunguza na kuondoa maudhui yasiyokubalika haraka iwezekanavyo. Hatua za kuondoa maudhui hayo zifanyike kwa hiari mara moja pale wanapobaini bila ya kusubiri malalamiko kutoka kwa walengwa au waathiriwa ama watu wengine.

vii) Iwapo wahariri au watayarishaji wa maudhui mtandaoni hawachukui hatua mapema ya kusimamia au kurekebisha maudhui ya mtu mwingine, wanaweza kufikiria kuanzisha utaratibu wa kabla au wa haraka wa kurekebisha mada maalumu zitakazoweza kusababisha maoni mengi muhimu au yasiyofaa. Hivyo, wahariri wanaweza kuzuia maudhui na maoni ya mtu mwingine kuchapishwa mtandaoni.

viii) Wahariri au watayarishaji wa maudhui mtandaoni ni lazima wawe na sera maalumu na taratibu za kutambua au kubainisha na kuondoa haraka maudhui ya ngono au picha, ama video mbaya zinazothiri faragha na utu wa watu walioathiriwa au kuguswa.

## 2.0. Taratibu za taarifa na uchukuaji wa hatua

i) Wahariri au watayarishaji wa maudhui mtandaoni watumie taratibu zinazofaa kwa ajili ya kupitia maoni ya umma au ripoti zinazohusu taarifa zinazokiuka sheria au zisizoruhusiwa na zinazokiuka sera za tovuti. Walalamikaji wapate uthibitisho kuwa taarifa zao zinashughulikiwa.

ii) Kisheria, wahariri au watayarishaji wa maudhui mtandaoni ni lazima wachukue hatua kuhusu malalamiko haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia masharti ya sheria na kanuni zinazohusika. Hata hivyo, kutokana na sababu maalumu, muda wa kushughulikia unaweza kuongezwa kwa matukio ambayo ni tata kwa mtazamo wa kisheria au kimaadili.

iii) Wahariri wasitishe kwa muda kidogo maudhui ambayo yanalalamikiwa na yanayohitaji kuangaliwa zaidi. Pia, wajitahidi kuwasiliana na waandishi wa maudhui hayo na kuwaalika waje watoe maoni yao kuhusu malalamiko yaliyopokewa. Wahariri wanaweza kuyarudisha maudhui waliyositisha baada ya kuridhika kuwa ni sahihi na ni kwa maslahi ya umma.

iv) Wahariri washughulikie maudhui ya mtu mwingine yasiyo na jina kwa uangalifu mkubwa. Kutokuwa na jina ni haki itakayowahusu watu wenye sababu maalumu, kwa mfano watoto au waathiriwa wa ugomvi au makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. Kwa kawaida wahariri na watayarishaji wa maudhui ya mtandaoni wawatarajie wachangiaji wengine wote kuwa wawazi na kutoa mawasiliano. Wanaweza kuzuia kwa muda au moja kawa moja watumiaji wanaojulikana na wasiojulikana kwa majina wanaokiuka mara kwa mara miongozo ya jamii au kulazimisha taarifa zao kupitiwa na kupunguzwa kabla ya kuchapishwa.

v) Wahariri wanaweza kuweka sheria zinazokataza matumizi ya nafasi ya maoni kwa shughuli za biashara au kujipatia faida, pamoja na kutumia matangazo yasiyo ya moja kwa moja au ya siri kwenye nafasi hiyo.

## 3.0. Matumizi ya taarifa ya mtu wa tatu kutoka kwenye mitandao ya kijamii au iliyotoka kwa umma

Picha binafsi, video au taarifa zilizoandikwa na kuchapishwa kwenye mitandao ya kijamii zinahesabiwa kuwa ni miliki ya umma na matumizi yake kwa vyombo vya habari kwa umma huziwezesha kutumiwa na hadhira pana. Uwezekano wa kupata picha kutoka mitandao ya kijamii au kurasa binafsi hakuzuii vyombo vya habari kutekeleza wajibu wao wa kufanya kazi kwa uangalifu. Maslahi ya umma katika uchapishaji wa taarifa ya namna hiyo yalinganishwe dhidi ya haki za faragha au kuwalinda watoto wadogo. Uchapishaji wa picha kwenye mitandao ya kijamii usisababishe kuhesabiwa kuwa ni ridhaa ya chanzo cha asili cha uchapishaji kwenye maeneo mengine au vyombo vya habari. Kutokana na hali hiyo, vyombo vya habari vya mtandaoni:

i) Vizingatie athari ya kutumia aina hiyo ya taarifa binafsi na makala, hasa kuhusiana na matukio ya kusikitisha kama vile misiba. Athari zinazohusu hakimiliki ni lazima zizingatiwe.

ii) Vichunguze kwa umakini na kuhakiki kujua uhalali wa picha na video zilizochukuliwa kutoka kwenye mitandao ya kijamii.

iii) Viwe makini daima hasa kuhusu hatari za kuchapisha picha zinazoonyesha tabia mbaya au tabia zisizokubalika kwa jamii au zinazokinzana na jamii. Vyombo vya habari mtandaoni

vihakikishe vinachukua tahadhari ili kuepuka kuwa vyombo vya kuhamasisha au kuhalalisha ukiukaji wa sheria kwa ujumla.

iv) Vichukue tahadhari kwa taarifa zenye mwingiliano kutokana na ushindani, uhusiano wake na zenye mkanganyiko.

## 4.0. Maoni/mrejesho

Watayarishaji wa maudhui mtandaoni wawape nafasi watazamaji kutoa maoni yao kuhusu habari au malalamiko au makala zao. Hata hivyo, mfumo utazuia moja kwa moja taarifa zinazotumia lugha chafu.

## 5.0. Uondoaji au uzuiaji wa maudhui

Ili kuepusha ujumbe usio na staha, wahariri wanatakiwa kuondoa au kuzuia ujumbe, picha au taarifa ndani ya saa mbili tangu kuwekwa mitandaoni kwa zisizozingatia sheria.

## 6.0. Hakimiliki

Kwa mujibu wa sheria za Tanzania, misingi ya hakimiliki inatumika kwa ukamilifu kwenye vyombo vya habari mtandaoni. Kuendelea kurudia kuchapisha maudhui na taarifa nyingine zilizotayarishwa na vyombo vya habari vingine bila ya ruhusa yao au kutaja chanzo kwa ukamilifu ni ukiukaji wa hakimiliki na huhesabiwa kuwa ni uvunjaji wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari. Aidha, nukuu ya maudhui ya mtu mwingine ionyeshe wazi chanzo au mwandishi wake wa awali na kufuata masharti mengine ya sheria ya hakimiliki.

## 7.0. Wizi wa maandishi

Vyombo vya habari mtandaoni visihusishe au kuruhusu kushirikiana taarifa, mawazo na kazi za watu wengine bila ya kuonyesha chanzo cha awali (kutoa shukrani) kwa usahihi. Wizi huu ni kunukuu maneno moja kwa moja kutoka vyombo vingine vya habari bila ya kutaja na kushukuru chanzo.

## 8.0. Kutaja chanzo

Vyombo vya habari mtandaoni viheshimu hakimiliki na matumizi ya hakimiliki pamoja na matumizi ya haki ya maudhui. Daima kwa kufanya hivyo ni kuwapa wahusika sifa na shukrani sahihi

kwa kazi zao.

## 9.0. Kulinda haki ya maudhui

Vyombo vya habari mtandaoni vidumishe udhibiti wa maudhui viliyoyatayarisha na kuweka miongozo kwa ajili ya kutaja na kushukuru sambamba na masharti kwa watumiaji kuboresha maudhui wanayoyatayarisha. Pia vitaomba ruhusa kabla ya kushirikisha na kutumia tena maudhui yasiyokuwa yake na vitaheshimu masharti ya hakimiliki wakati wa kuunganisha au kutumia tena maudhui ya watu wengine. Hatua hiyo itatumika pia kwa picha mbalimbali zikiwemo video, michoro, matangazo ya sauti ya moja kwa moja (podikasti) na picha maalumu.

## 10.0. Kulinda faragha ya maudhui

Vyombo vya habari vya mtandaoni vilinde faragha ya maudhui yake na kuweka sera ya wazi kuhusu ruhusa ya kutumia au kutumia tena maudhui yake. Aina ya taarifa ya kulindwa na sera ya kuongoza au kuelekeza faragha itakuwa kwa mujibu wa sheria za nchi na kanuni zinazosimamia udhibiti wa taarifa mitandaoni.

## 11.0. Nyaraka za mtandaoni, uchapishaji tena maudhui ya mtu mwingine

Vyombo vya habari mtandaoni ni lazima vitunze nyaraka za maudhui yao viliyochapisha kwa ukamilifu kadiri iwezekanavyo. Nyaraka za kudumu za taarifa zinazochangia katika uhifadhi wa kumbukumbu za historia zihaririwe au kuondolewa tu kwa sababu maalumu, kama vile amri ya mahakama au kuendelea kuchapishwa au kama kuchapisha kunaweza kuhatarisha zaidi ustawi na usalama wa watoto au uadilifu wa kimwili na kiakili wa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, au iwapo uchapishaji wa awali haukuwa sahihi ama umesitishwa kutokana na kukiuka maadili. Kama kawaida kila uhariri ni lazima uambatane na maelezo kwenye ukurasa unaohusika. Wahariri wanaweza kuchagua kutotaja majina ya vyanzo badala ya kuondoa maudhui yanayohusika pale inapofaa.

Misingi ya hakimiliki inatumika kwa ukamilifu katika machapisho ya mtandaoni kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Uchapishaji wa maudhui yaliyorudiwa na taarifa nyingine zilizotayarishwa na vyombo vya habari vingine, bila ya ruhusa zao au kushukuriwa

inavyopasa, ni ukiukaji wa hakimiliki na huhesabiwa kuwa ni uvunjaji mkubwa wa maadili ya uandishi wa habari. Aidha, kunukuu vyovyote maudhui ya mtu mwingine uonyeshe wazi chanzo au mwandishi wa makala au taarifa husika na kufuata masharti mengine ya sheria ya hakimiliki.

### 12.0. Utangazaji biashara mtandaoni

Vyombo vya habari mtandaoni visitangaze au kuruhusu matangazo yenye maudhui yanakwenda kinyume na kanuni hizi za maadili.

### 13.0. Kanusho

Vyombo vya habari mtandaoni vitakuwa na kanusho lililoambatishwa kwenye akaunti za wachangiaji kwa madhumuni ya kutofautisha mawazo binafsi na wachangiaji wa maudhui wanayoshirikishana kwa niaba ya jukwaa lake.

# SURA YA NNE

## MISINGI INAYOTUMIKA KWA WAMILIKI WA VYOMBO VYA HABARI NA WACHAPISHAJI

Wamiliki wa vyombo vya habari au wachapishaji wana mamlaka makubwa kwa machapisho, vituo vya redio, viyup vya televisheni au machapisho ya mtandaoni wanavyomiliki. Ili kudumisha uthabiti wa uhuru na weledi, wamiliki wa vyombo vya habari au wachapishaji wazingatie:

### 1.0. Uhuru

Wamiliki wa vyombo vya habari wasitumie mamlaka yao kufanya uamuzi kwa kutoa upendeleo au kudhibiti uhuru wa wafanyakazi wa vyombo vya habari. Uteuzi wa wahariri na waandishi wa habari, upandishaji vyeo, malipo, mishahara na fursa ya mafunzo vitazingatia zaidi sifa na sio vitu vingine kama vile uhusiano wa kifamilia au wa kisiasa.

### 2.0. Usalama na muda wa ajira

Wamiliki wa vyombo vya habari na wachapishaji ni lazima wahakikishe kuwa wahariri na waandishi wa habari wanafurahia usalama wa mikataba ya muda  wa ajira zao na wanaweza kuachishwa kazi tu kwa makosa maalumu kama vile tabia mbaya au kukosa weledi baada ya uchuguzi. Wasiingilie kazi za uhariri na waheshimu uamuzi wa waandishi wa habari kwenye ajira zao.

### 3.0. Msukumo usio wa lazima au ushawishi

Wasikandamize au kupotosha taarifa ambazo umma una haki ya kujua kwa sababu ya nguvu isiyo ya lazima au ushawishi kutokana na maslahi ya kibiashara, kisiasa, kijamii, kiuchumi au kidini.

### 4.0. Unyanyasaji wa kijinsia

Wamiliki wa vyombo vya habari watunge sera za unyanyasaji wa kijinsia zitakazowalinda wanawake na wanaume dhidi ya mashambulizi ya kijinsia. Sera hizi ziwe na taratibu za kuziwezesha kufanya kazi na kuzifanya zipatikane kwa watumishi wote.

## 5.0. Kulipia taarifa

Wamiliki wa vyombo vya habari na wachapishaji watunge sheria kali za kuzuia uchapishaji au taarifa ya tahariri au kuacha ama kubadili hoja muhimu kwa ajili ya malipo ya fedha au zawadi na tunzo. Hata hivyo, hii haihusu matangazo au makala za watangazaji. Vyombo vya habari vitofautishe maudhui ya tahariri, matangazo au makala za watangazaji.

## 6.0. Mgongano wa maslahi

i) Wamiliki wa vyombo vya habari wasitumie uhusiano wao kushawishi vyombo vya habari kuhatarisha nafasi zao za kimaadili na viwango vya kitaaluma.

ii) Wamiliki wa vyombo vya habari wawaache waandishi wa habari kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu kazi zozote za kitaaluma na kwa vyovyote vile taarifa za wahariri zizingatie kile ambacho mhariri anaamini kuwa ni kwa maslahi ya wasomaji, watazamaji au wasikilizaji na si kwa wamiliki au matakwa na maslahi ya wachapishaji.

## 7.0. Weledi wa kitaaluma

Wawawezeshe wafanyakazi wao kuongeza weledi wa kitaaluma kwa mafunzo na masomo zaidi. Vilevile, wamiliki wa vyombo vya habari wahakikishe kuwa wafanyakazi wao wanawezeshwa kuhusu ubunifu mpya katika tasnia ya habari.

## 8.0. Nguvu au vitisho

Wamiliki wa vyombo vya habari au wachapishaji wawalinde wafanyakazi wao wanaotishiwa au kushambuliwa, zana za kazi au ofisi zao mpaka vitisho hivyo vitakapopita.

## 9.0. Kurudisha fadhila kwa jamii

i) Wamiliki wa vyombo vya habari watimize wajibu wao kwa kurudisha fadhila kwa jamii, inayomaanisha kuwa vyombo vya habari kutilia mkazo katika kuhamasisha ustawi wa jamii zaidi kuliko maslahi ya kibiashara.

ii) Wamiliki wa vyombo vya habari wasiingilie au kudharau kwa sababu yoyote ile mamlaka ya vyombo vyao ikiwemo

ya kuifuatilia Serikali na vituo vingine vyenye ushawishi na mamlaka kwa niaba ya umma.

## 10.0. Uchunguzi

Wamiliki wa vyombo vya habari wakubali uchunguzi wa mambo yao wenyewe. Uchunguzi huu usiagizwe na Serikali, bali kupitia vyombo vilivyoundwa na vyombo vya habari vyenyewe, kama vile Baraza la Habari Tanzania (MCT) vinavyozingatia zaidi uwajibikaji kidemokrasia kwa umma waouchapishia machapisho.

## Marejeo


Code of ethics and conduct for South African Print and Online Media retrieved from; https://sanef.org.za/wp-content/uploads/2019/02/Press-Ombusman-Decoding-the-Code-January-2019.pdf

Code of ethics and conduct for Namibian Print, Broadcast and Online media-retrieved fromhttps://www.namibian.com.na/public/uploads/documents/5922bc565ea0f/code%20of%20ethics%20online.pdf

Code of conduct for the practice of journalism in Kenya, 2013, Kenya Media Council

Colón, A. (2017). You are the new gatekeeper of the news. [online] The Conversation. Available at https://theconversation.com/you-are-thenew-gatekeeper-of-the-news-71862 [accessed 05/07/2020].

Dar es Salaam Declaration on Editorial Freedom, Independence and Responsibilities (DEFIR), Media Council of Tanzania publication, 2011.

Díaz-Campo, J., &Segado-Boj, F. (2015). Journalism ethics in a digitalenvironment: How journalistic codes of ethics have been adapted to theInternet and ICTs in countries around the world. Telematics andInformatics, 32 (4), 735-744.

Edelman. (2017). 2017 Edelman Trust Barometer- Global Results. Available at https://www.edelman.com/global-results/ [accessed 25/06/2020].

Guidelines for Tanzania Online Content Producers - English Version, July 12, 2020

Hall, J (n.d), Online Journalism: A Critical Primer, London: Pluto Press.

https://www.mediacouncil.or.ke/en/mck/index.php/code-of-conduct-for-the-practice-of-journalism-in-kenya [accessed 22/06/2020].

Mackay, A. (2004), The Practice of Advertising, London: Butterworth-Heinemann.

Mamishev, A. and Williams, S. (2009), Technical Writing for Teams: The STREAM Tools Handbook, Institute of Electrical and Electronics Engineers, John Wiley & Sons. Inc., Hoboken, p.128

Manovich, L. (2003), New Media from Borges to HTML, In: Noah Wardrip-Fruin& Nick Montfort (eds), The New Media Reader, Cambridge, Massachusetts, 13-25.

Media Services Act 2016, Information Services Part 11

https://www.tanzania.go.tz/egov_uploads/documents/THE_MEDIA_SERVICES_ACT,_No_sw.pdf [accessed 20/06/2020].

Paul Kimumwe (2014). Media Regulation and Practice in Uganda: A Journalists Handbook, 2014 Clearmark Publishers, Kampala.

Posetti, J. (2017). Protecting Journalism Sources in the Digital Age (UNESCO) http://unesdoc.unesco.org/images/0024/002480/248054E.pdf [accessed 01/07/2020].

Randall, D. (2000), The Universal Journalist, Sterling Virginia: Pluto Press.

Sambrook, R (2012): Delivering Trust: Impartiality and Objectivity in the Digital Age

https://reutersinstitute.politics.ox.ac.uk/sites/default/files/2017-11/Delivering%20Trust%20Impartiality%20and%20Objectivity%20in%20a%20Digital%20Age.pdf[accessed 28/06/2020].

Schivinski, B and Dąbrowski, D. (2014), The Effect of Social-Media Communication on Consumer Perceptions of Brands, Journal of Marketing Communications: 2–19.

Second Schedule of the Media Council Act2013: Code of Conduct for the Practice of Journalism in Kenya

Tara K. Harper (2004), On Publishers and Getting Published, Retrieved 28 May 2010.

The BBC's Editorial Values and Standards 2020

https://www.bbc.co.uk/editorialguidelines/guidelines/conflicts-of-interest [accessed 15/06/2020].

UNESCO (2018). Journalism, 'Fake News' & Disinformation

https://en.unesco.org/sites/default/files/journalism_fake_news_disinformation_print_friendly_0.pdf [accessed 01/07/2020].

Vaughn, S. L. (ed) (2008), Encyclopedia of American Journalism, New York: Routledge.

Published by Media Council of Tanzania (MCT)
P.O.Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2775728/2771947
Mob: +255-784314880
E-mail: media@mct.or.tz Website: www.mct.or.tz

**ISBN: 978 - 9987 - 710 - 95 - 9**

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA